LEARNING BY EAR EPISODE – Girls
Episode 6: Sport
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

Intro:
Ni wakati mwingine tunapokutana tena kwenye makala haya ya Jifunze Kwa Kusikiliza. Leo hii Bibiy na wenzake wanapambana kwenye mchezo wa mpira wa miguu na timu ya wavulana. Je wasichana hawa wanajiandaa vipi katika mchezo wa leo? Karibu kwenye sehemu ya sita ya mchezo huu wa kusisimua kwa jina Kabumbu.

CHARACTERS:
Anchor: Intro / Autro
Bibiy........Main Character
Alma.......same character
Rossie.......same character
PE. Teacher/Coach............Woman (Adult)
Kibegu......same character
Timo.........same character
Provincial Sports Officer.......Male (Adult).

Sign Tune

SCENE ONE:
(Katika uwanja wa shule wasichana na mkufunzi wao, sauti ya firimbi na mpira ukipigwa inasikika huku sauti za wasichana pia zikisikika. etc.)

COACH: (anapuliza firimbi) Ndio wasichana wangu nimewaita hapa mkusanyike karibu na mimi kwa kuwa nataka kuwaeleza mambo ya muhimu. Ningemuomba kila mmoja wenu anisikilize kwa makini sana. Naam nyote hapa mnajua kwamba hii ndio mara yetu ya mwisho kufanya mazoezi kabla ya mchuano mkubwa kati ya timu yetu na ile ya wavulana. Vilevile ningependa kuchukua fursa hii kuwapongezeni sana kwa juhudi mliyo onyesha wakati wote wa mazoezi na ninatarajia kuwa

juhudi yenu itazaa matunda kwa kuwafunga wavulana na hivyo kutupa ushindi mkubwa ambao tunautarajia kwa hamu na nina imani kubwa kuwa ushindi huo tutaupata.
(wasichana wanapiga makofi)

BIBIY: ndio ndio! (wasichana wanaitikia).. Ndio tunaweza (Bibiy anarudia tena na wasichana wanaitikia tena).

ALMA: Mwalimu nauliza mechi yetu tutaichezea wapi? Hapa kwenye huu uwanja wetu au itakuwa wapi?

COACH: Swali zuri hilo Alma..Eenh!..Afisa wa mkoa anaehusika na michezo amenifahamisha kuwa mechi hii ni muhimu sana kwa hivyo imependekezwa kuwa tutachuana na wavulana kwenye uwanja wa michezo wa taifa.. Sasa basi nataka kuwafahamisha kuwa uwanja huo ni mkubwa kuliko huu wetu ambao mmeuzoea na kwa hivyo afisa michezo leo hii ameturuhusu tukafanye mazoezi yetu huko ili mpate uzoefu wa uwanja huo kabla ya mchuano wenyewe…ndio maana mwalimu mkuu ametuandalia usafiri ili tuelekee huko. Kwa sasa nataka kila mmoja wenu achukue mfuko wake wa mazoezi, kwa utaratibu tuingie kwenye gari lile pale tuelekee uwanja wa taifa.
(Wasichana wanafurahia)

ROSSIE: Mimi nakwambia nina hamu sana ifike wakati wa mchuano nataka tuwaonyeshe wavulana maajabu kuwa hata na sisi mpira tunaujua..maanake nadhani wao wanatudharau sana wanafikiria sisi magoigoi na wala hatujui kucheza football.

BIBIY: (anacheka) watashangaa kwani kama bado wapo wanaofikiria kuwa hatuwezi kulisakata kabumbu mbona bado wako usingizini! Wakija kuamka itakuwa tayari wamepitwa na mambo..Wakati umefika sasa wavulana watambue kuwa wasichana ulimwenguni kote wamepiga hatua sawa na wavulana..Ni juzi juzi tu tuliwashinda vibaya kwenye mjadala na pia tuliwaonyesha vumbi kwenye mashindano ya mbio shuleni..NDIO NDIO! (Wasichana wanaitikia) NDIO TUNAWEZA x2.

ALMA: Si hayo tu hata kwenye masomo ya hesabu, sayansi na mengineyo pia tumeamka tunakwenda nao sambamba na hata kuwaacha nyuma. Yaani watatuchoka..sasa watungojee uwanjani watakiona kivumbi!

COACH: OK. Ok basi wasichana, moja mbili tatu tuanze kuingia ndani ya gari..enhee endeleni kuingia.. kumi, kumi na moja, kumi na mbili. Nafikiri sote tumekamilika au vipi? (Wasichana wanaitikia: Yeaah! tumekamilika) Sawa dereva tunaweza kuondoka. (Gari linaondoka).

MUSIC

SCENE TWO:
TIMO: Kibegu, vipi rafiki yangu tunajitayarisha vipi kusherehekea ushindi wetu wa rahisi dhidi ya wasichana! Maanake huo ni ushidi wa kupewa wala hatuhitaji kutumia nguvu nyingi.

KIBEGU: Hiyo ni kweli rafiki yangu. Ni wazi kuwa ushindi huo ni wetu hata mtu ukiwa usingizini utajibu tu ukiulizwa ni nani atakae shinda kati yetu na wasichana.. hilo halina upinzani ikiwa mchezo ni football si kila mtu anajua football ni ya kina nani?..Timo football ni mchezo wetu ni mchezo wa wanaume, wasichana wao wanajua kusema tu..maneno mengi tu ndio yao, lakini wajue kuwa kabumbu sio sawa na mjadala..tutawaonyesha kuwa kuzungumza sio sawa na kucheza football. Watakiona cha mtema kuni maanake hatuna haja ya kutumia nguvu nyingi tutawaonyesha jinsi mpira unavyochezwa halafu tukishawashinda tutaandaa Party kubwa kisha tuwaalike waje washerekee ushindi wetu.

TIMO: Yeah, hilo ni wazo zuri tena basi kwenye hiyo Party wao ndio watakuja kutayarisha vyakula. Hawa wasichana wanatuchezea sana hawajui kuwa sisi ndio ma-star wenyewe, akina E'to na Drogba eeh! ndio sisi. Nakwambia itakuwa kichekesho siku hiyo, kwa kuwa kila mmoja kwenye timu yetu atafunga bao lake mpaka goal keeper wetu! Bibiy na timu yake

watakwenda nyumbani huku wamerowa machozi chapa chapa…magli kumi na moja tutawafunga bila ya huruma.

KIBEGU: Timo (Anacheka ha ha ha!), Hiyo ni kali, rafiki yangu Loo! hiyo ndio yenyewe maanake kila mmoja wao atabeba goli lake. Ha, ha, ha.

TIMO: Kibegu, twende zetu rafiki yangu.. wenzetu wanatusubiri uwanjani..mazoezi karibu yataanza twende zetu bwana…usiwafikirie sana hao wasichana, wanataka kucheza na moto wajue wataungua, tangu lini wasichana wakacheza football?

MUSIC

COACH: (Anapiga firimbi) OK! wasichana wangu wazuri mazoezi hayo yametosha kwa leo..njooni hapa .
(Wasichana wanahema kwa kukimbia)

BIBIY: Mazoezi yetu yalikuwa mazuri mno leo..nina hakika mmepata nafasi nzuri ya kuuelewa uwanja huu ambo tunatarajiwa kujibwaga hapa mwishoni mwa wiki kuwaonyesha wavulana kuwa tunaweza..kwa kweli uwanja wenyewe ni mkubwa lakini nina imani kuwa katika uwanja huu tutaandika historia na kuwa timu ya kwanza ya wasichana kuwahi kuwa fungisha virago wavulana katika mpira wa miguu au manasemaje?

BIBIY: Ndio Ndio! (Wasichana wanajibu) Ndio Tunaweza x2.

ROSSIE: Mwalimu kwa kweli uwanja huu ni mkubwa na pia ni wa kisasa lakini hata nasisi tutajitahidi mpaka tuwafunge wavulana..wazazi wangu pia wamesema watakuja kutazama mechi hiyo.

COACH: Oh! Ni vizuri sana.. very good. Wazazi ni kiungo muhimu katika kuwatia moyo watoto wao ili wajihusishe na michezo mbali mbali. Tafadhali nyote msisahau kuwaambia

wazazi wenu kuwa wasikose kabisa kuja kutushangilia..tunawahitaji sana siku hiyo. Mhh! Mbali na wazazi je nani anaweza kutuambia juu ya mtu mwingine ambae amekuwa kielelezo kwake ambae amemfanya awe na moyo wa kupenda michezo? Enhee! Rossie tuambie ni nani amekupa wewe changamoto?

ROSSIE: Mimi nimevutiwa na wana michezo wengi tu ambao wamekuwa kielelezo changu katika michezo hasa wanamichezo wanawake. Kwa mfano Yule mwanadada mkimbiaji Maria Mutola kutoka Mozambique au, Catherine Ndereba kutoka Kenya na wengine wengi.

ALMA: Mimi nimevutiwa sana na timu ya kandanda za wanawake ya Ujerumani ambao wamechukuwa ubingwa wa mpira wa miguu duniani. Labda hata na sisi siku moja tutashiriki katika michuano ya kombe la dunia.

COACH: Asaneni sana.. ni kweli michezo inavutia na ina uwezo mkubwa wa kuwashawishi vijana. Michezo inawafanya vijana kufikiria mambo ya kujiendeleza na pia inajenga hisia za kujiamini. Nami nikiwa mkufunzi wenu ninawashauri muongeze juhudi katika kila jambo na kuhakikisha kuwa mnafikia malengo yenu. Vilevile msisahau kuwa nyinyi ndio kilelezo kwa wasichana wenzenu.. Na la muhimu nataka muwe tayari kupambana na wavulana katika mechi ijayo bila uoga wowote.

BIBIY: Usiwe na wasiwasi mwalimu sisi tuko tayari kabisa na tuna uhakika wa kushinda.. kwa sababu tunajiamini.

COACH: Kwa hiyo washambuliaji wetu natumai mbinu mpya mmezihifadhi vizuri na mtazitumia na ikiwa hayo ni sawa basi tunatarajia mabao kadhaa.. Tumieni kila nafasi kufunga goli, kumbukeni msifanye mchezo wa kutaka kuonyesha kuwa mnaweza kuzuunguuka na mpira bure bure bila sababu..ukipata nafasi tu Shoot Goal!..jaribuni kukumbuka yale yote tuliyojifunza ..na basi hayo nafikiri yametosha, sasa tukusanye vifaa vyetu tayari kwa kuondoka.

MUSIC

SCENE THREE:
(Uwanjani…watu wanazungumza kwa kelele..sauti za matarumbeta, ngoma na nyimbo zinasikika.)

SPORTS OFFICER: Mabibi na mabwana ninafuraha tele kuwakaribisha katika mashindano haya muhimu kabisa. Leo kwa mara ya kwanza katika historia ya mji wetu wasichana watapambana na wavulana katika mpira wa miguu..kwa hiyo tunatarajia kuona mchezo wa hali ya juu baina ya timu hizo mbili.
(Watu wanashagilia, makofi,ngoma na tarumbeta zinasikika)
Mchuano huu wa leo kati ya timu ya wasichana na wavulana unaungwa mkono na wale wote wanaopenda michezo na wanaojali kuendeleza michezo kwa vijana wetu kwa kuwa tunatilia maanani swala la kuufanya ulimwengu wetu kuwa ni mahala bora pa kuishi. Ninawakaribisha wote kwa moyo mkunjufu na ninawatakia furaha tele katika kuangalia mchuano huu wa leo… enjoy the game.
(Makofi)

COACH: Sasa wasichana wangu wakati umefika. Bila shaka mnajiamini, ujuzi mnao na la muhimu mnalo paswa kufikiria ni kuwa tumekuja hapa kushinda mechi hii na wala sio vinginevyo..Nia na sababu ya kutaka kushinda mchuano huu tunayo na sote tunajua kuwa tunataka kuwaonyesha wavulana na ulimwengu mzima kuwa hata wasichana wanaweza kucheza football kama wavulana! Ana pengine hata zaidi ya wavulana OK! – Nawatakieni kila la kheri.
(Sauti za mashabiki zinasikika)......

BIBIY: Hey jamani muhimu tuseme sala yetu...(Wote Pamoja).

Tunasimama Pamoja
Tumekata kauli Pamoja
Kuufukuza mprira kwa Pamoja
Hadi ndani ya wavu wa wavulana

BIBIY: Ndio Ndio! (Wasichana wanaitikia) Ndio Tunaweza. x2 (Kelele za mashabiki zinasikika).......

TIMO: Jamani wakati wa kuwonyesha watu show umefika. Na kama tulivyokuwa tumezungumza kwamba hawa wapinzani wetu tuwabandike kila mmoja bao lake ili aende nalo nyumbai, basi wembe ni ule ule. Mimi Kapteni wenu nasema tucheze mpira wa uhakika maanake mnaona jinsi gani uwanja ulivyojaa watu..La muhimu tunalopaswa kukumbuka ni kuwa hatutaki kushindwa mechi hii na wasichana..Je tuko tayari? (Wavulana wengine wanaitikia: yeah! Tuko tayari kapteni)

KIBEGU: Rip, Rip! (wavulana wanaitikia: 'hurray!' x2) Captain eeh, Unaitwa kule. Nafikiria refarii yuko tayari kurusha sarafu..leo ni leo timu bora itajulikana! .
(Firimbi inalia mchezo unaanza).
Sound Effects......Mtangazi wa mpira, sauti za amshabiki) approx. 25 to 30 seconds – halafu.. Gooooaaaaall!!!.
(Firimbi inalia mpira umekwisha)

COACH: Wow! Hata siamini. Wasichana wangu jamani wameshinda..loo ! wamewashinda wavulana . Ha, ha! Tumefunga mabao mawili kwa moja. nifuraha iliyoje! (Vifijo.kelele,tarumbeta, ngoma etc.)

BIBIY: He! he! he! Wako wapi wavulana? Loo wamekimbia, wamejificha! Oh, nina furaha kweli….leo ni siku ya furaha maishani mwetu! Tumeshinda..tumewafungisha virago wavulana!…He he! Tumewaning’iniza vichwa chini miguu juu.

COACH: Ooh njooni hapa wasichana wangu njooni tufurahi pamoja..tufurahie ushindi wetu. Je tumewashinda kina nani? (wasichana wanaitikia) wavulana!

ROSSIE: Bibiy Umetupa ushindi rafiki yangu magoli yote mawili kutoka kwako! Ooh nina furaha sana! Sitaisahau siku hii maisha.

ALMA: Nakwambia vile wavulana walivyokuwa wakituangalia.. kwanza tulivyoingia uwanjani Hee walikuwa hundred percent sure kuwa watatufunga. Walijiamini tu kuwa aah hawa ni wasichana kwa hivyo tutawafunga! Ng'o hawakutupata.

BIBIY: Wajua walipoanza kufunga tu wakadhani basi ndio mwisho lakini ile pasi kutoka kwa Gladys ndio iliyonifanya nikarudisha lile bao la kwanza halafu na lile bao la pili ni pale Rossie aliponipasia mpira nakwambia nilimpita Kibegu nikauinua mpira juu ya kichwa cha goal keeper wao na hapo goli letu la pili likaingia wavuni.

COACH:Ooh wasichana wangu kwa kweli mmecheza mpira wa hali ya juu sana kama vile vile tulivyo jifunza mbinu mpya mmefuata maagizo yote sawa sawa kwanza mkawazubaisha hadi wakaacha kulilinda lango lao na hapo ndipo walipo ingia mtegoni. Sasa twendeni tukapokee kombe letu ni wakati wetu wa kuringa.

MUSIC

SCENE FOUR:
TIMO: Kibegu rafiki yangu kulitokea nini mbona tumeshindwa kiurahisi vile na wasichana! Hata siamini..au wametumia uchawi?

KIBEGU: Hapana Timo, hamna uchawi hamna lolote lakini hata sijui ilikuwaje.. ni wapi tulipokosea sisi?

TIMO: Hapana mimi nafikiria Yule refarii aliwapendelea wasichana. Si unaona alitunyima penalty tatu waziwazi wakati wasicana walipotuchezea rafu hiyo ilikuwa ni plani ya kuwapendelea tu!.

KIBEGU: Mimi sifikirii hivyo. Labda baadhi yetu hatuku uangalia mpira vyema. Lakini bwana wale wasichana wanacheza mpira mzuri kweli kweli, lazima tukubali hilo.
TIMO: Basi Kibegu, nyamaza naona wanakuja.

BIBIY: hata msinyamaze endeleeni tu kuzungumza tumesikia kila kitu. Ni lazima mkubali kuwa sisi mpira tunaujua na kushinda nyinyi kwa sababu mazoezi ndio mafanikio ya kila jambo kimombo wanasema practice makes perfect!

ALMA: Ndio! Yote hayo ni kwa sababu sisi tunajiamini.miaka michache iliyopita tulikuwa hatujui kucheza foot ball hata kidogo.

KIBEGU: Mimi ni mmoja kati ya wale watu ambao wanafikiria kuwa wasichana hawawezi kucheza kabumbu loo kumbe nimenoa!

BIBIY: Ni kweli lazima ubadili mawazo hayo na wakati ni sasa. Ujue kuwa wasichana wana uwezo sawa na wavulana.

TIMO: Bibiy, bado nashindwa kuamini kuwa mmetushinda.

BIBIY: Timo mambo bado tunapanga kupambana nanyi tena kwenye mbio na michezo mingine pia.

ROSSIE: hata hivyo tunawaalika kwenye Party yetu ya ushindi.

BIBIY: Ndio wageni wengi watahudhuria afisa michezo na wazazi wetu piawatakuja, tunataka mtusaidie kazi kidogo!

KIBEGU: Mnataka tuwasaidie vipi?

BIBIY: Tunataka msafishe ukumbi na kupanga meza pamoja na kubeba vinywaji.

TIMO: Halafu baada ya hapo?

ALMA: Mtatusaidia pia kuondoa kila kitu na kusafisha ukumbi tena.

KIBEGU: Asanteni kwa mualiko na msiwe na wasiwasi tutawasidia kama mlivyo taka.

TIMO: Na wakati huo tutapanga tena mechi nyingine.

BIBIY: Hamna shida sisi tuko tayari kuwashinda wakati wowote.. jamani sasa tuondokeni ili tukajitayarishe kwa hiyo Party. Rossie utavaa nini?

ROSSIE: Itabidi usubiri hadi utakaponiona huko kwenye Party na wewe je mbona huniambii utavaa nini?

BIBIY: Usijali rafiki yangu na mimi pia nataka kuwashtua..jamani kwaherini!

MUSIC....

Autro: Wavulana hawakutarajia kufungwa na wasichana lakini mambo yamegeuka na wasichana wamechukua ushindi. Mpaka hapo ndio tumekamilisha mchezo kwa jina Kabumbu katika sehemu ya sita ya makala za Jifunze Kwa kusikiliza. Mwambie rafiki yako ausikilize mchezo huu au wewe unaweza pia kuusikiliza tena kupitia kwenye tovuti yetu. HYPERLINK "http://www.dw-world.de/lbe" www.dw-world.de/lbe . Jiunge na msichana Bibiy pamoja na wenzake wiki ijayo katika sehemu ya saba ya Jifunze Kwa Kusikiliza mpaka wakati huo kwa heri kwa sasa.

END